

Je, ni matatizo yapi yanayotokana na ujauzito katika umri mkubwa?

By SW - Melkisedeck Shine · April 17, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Kwa wanawake wenye miaka zaidi ya 35 uwezekano wa kupata matatizo ya kiafya wakati wa ujauzito au wakati wa kujifungua ni mkubwa zaidi kuliko wanawake kati ya miaka 20 na 35. Matatizo ni mengi zaidi kama mama ameshakuwa na watoto wengi. Baada ya kuzaa mimba tano au zaidi, misuli ya mfuko wa uzazi hulegea. Hivyo hufanya mama kutokwa na damu nyingi, kuwa na uchungu wa muda mrefu na kuchanika kwa mji wa mimba. Matatizo mengine ni mtoto kukaa vibaya tumboni na kuwa na watoto wakubwa. Wanawake wa umri mkubwa ambao wamekuwa na idadi kubwa ya mimba za karibukaribu (za kufululiza) wanakabiliwa na uwezekano mkubwa wa kufariki wakati wa ujauzito na wakati wa kujifungua.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25990>